# Ripoti ya Bomani




policy forum

**Taarifa fupi ya Kamati ya Rais ya Kuishauri Serikali kuhusu**

## Usimamizi wa Sekta ya Madini

# TAARIFA FUPI YA KAMATI YA RAIS YA KUISHAURI SERIKALI KUHUSU USIMAMIZI WA SEKTA YA MADINI-JUZUU NA. 2

Kimetayarishwa na:
Lina W. Magoma- Policy Forum Secretariat

Kimehaririwa na:
Reginald Martin- Legal and Human Rights Centre (LHRC)
Gertrude Mugizi- Policy Forum Secretariat

Kimechapishwa na Policy Forum 2008.

Kitabu hiki sio tafsiri ya neno kwa neno ya 'Taarifa ya Kamati ya Rais ya Kuishauri Serikali Kuhusu Usimamizi wa Sekta ya Madini' Juzuu Namba 2, hivyo tunashauri kisomwe pamoja na Taarifa hiyo husika kwa rejea.

Mchoraji: Nathan Mpangala

ISBN 978-9987-9157-3-6

# Yaliyomo


Wajumbe wa Kamati:- ............ iv

**Sura ya kwanza ............ 1**

1.1 Utangulizi ............ 1

1.2 Kuundwa kwa Kamati ............ 1

1.3 Majukumu ya Kamati ............ 2

1.4 Muundo wa Taarifa ya Kamati ............ 2

**Sura ya pili ............ 3**

2.1 Hali halisi ya sekta ya madini ............ 3

2.1.1 Kodi ya Mapato ............ 4

2.1.2 Kodi ya Ongezeko la Thamani (Value added Tax- VAT) ............ 5

2.1.3 Ushuru wa Forodha ............ 5

2.1.4 Ushuru wa Bidhaa. ............ 6

2.1.5 Ushuru wa Mafuta ............ 6

2.1.6 Ushuru wa Stempu ............ 6

2.1.7 Kodi za Serikali za Mitaa ............ 6

2.2 Mikataba ya Madini: ............ 6

2.3 Matatizo ya wachimbaji wadogo; ............ 7

**Sura ya tatu ............ 8**

3.1 Maoni ya wadau: ............ 8

**Sura ya nne ............ 10**

4.1 Tathmini, maoni na mapendekezo ya kamati. ............ 10

4.1.1 Wajibu wa Serikali na mwekezaji; Mapendekezo: ............ 10

4.1.2 Sera ya Madini ya mwaka 1997; Mapendekezo:- ............ 10

4.1.3 Mapendekezo mengine kwenye Sheria ya Madini; ............ 11

4.1.4 Mamlaka ya Waziri kufuta Leseni; Mapendekezo:- ............ 11

4.1.5 Mamlaka ya Waziri kuingia mikataba; Mapendekezo: ............ 11

4.1.6 Kamati ya ushauri ya madini (MAC); ............ 12

4.1.7 Masuala ya Fidia; Mapendekezo: ............ 12

4.1.8 Utatuzi wa migogoro; Mapendekezo: ............ 12

4.1.9 Utozaji wa Mrabaha; Mapendekezo: ............ 12

4.1.10 Usimamizi wa sekta ya madini; Mapendekezo:- .............................. 13
4.1.11 Umiliki na ushiriki wa Serikali katika sekta ya madini; .................. 13
4.1.12 Mgawanyo wa mapato yatokanayo na madini;................................ 14
4.1.13 Mikataba ya madini;...................................................................... 14
4.1.14 Ulipaji wa fidia;- Mapendekezo:..................................................... 15
4.1.15 Wachimbaji wadogo; Mapendekezo:- ............................................ 15
4.1.16 Mchango wa Sekta ya Madini katika Maendeleo na huduma za jamii (Corporate Social Responsibility); Mapendekezo:- .......................... 16
4.1.17 Ajira na rasilimali watu; ................................................................ 16
4.1.18 Biashara ya madini; Mapendekezo:- ............................................... 16
4.1.19 Usimamizi wa mazingira; Mapendekezo: ....................................... 16
4.1.20 Uchenjuaji na usafishaji madini; Mapendekezo:- ............................. 17
4.2 Fungamanisho la sekta ya madini na uchumi; Mapendekezo:-...................... 17
4.3 Fungamanisho la sekta ya madini na sekta ndogo ya umeme. Mapendekezo:-17

**Sura ya tano.......................................................................................... 18**
5.1 Hitimisho ........................................................................................... 18
Mkakati wa utekelezaji wa mapendekezo yaliyomo kwenye taarifa hii ........ 19

# Dibaji

Policy Forum tunayo furaha kuchapisha kitabu hiki ambacho kinatokana na 'Taarifa ya Kamati ya Rais ya Kuishauri Serikali Kuhusu Usimamizi wa Sekta ya Madini' Juzuu Namba 2.

Shukrani kwa Reginald Martin wa LHRC kwa ushirikiano wake wa hali na mali ikiwa ni pamoja na kutumia muda wake kuhakikisha anaihariri Taarifa hii fupi. Bila kumsahau mchora katuni wetu Nathan Mpangala.

Ni wazi kuwa taarifa nyingi za Kamati zinazoundwa huwa ni ndefu na hivyo kuwapelekea wananchi wa kawaida ambao ni wadau muhimu sana katika jamii kushindwa kusoma au kutoielewa kabisa kutokana na lugha inayotumika. Hii ilipelekea Policy Forum kuamua kuandaa tafsiri rahisi ya taarifa hiyo kwa kutumia lugha rahisi na vielelezo kama katuni.

Sote tunafahamu Tanzania imebarikiwa neema ya madini ya aina mbalimbali yaliyopo nchini pote. Lakini pamoja na kujaliwa wingi wa madini mbalimbali bado inaonekana kuwa sekta ya madini haichangii vya kutosha katika maendeleo ya nchi hasa ya kiuchumi na kijamii na pia kuonekana kuwa mikataba ya madini inapendelea zaidi kampuni kubwa za uwekezaji katika madini, ikiwemo usiri mkubwa wa mikataba hiyo.

Ni matarajio yetu kuwa tafsiri hii rahisi ya taarifa ya kamati ya madini itawasaidia watanzania wote kuelewa kinachoendelea katika sekta ya madini na mapendekezo ya kamati kama yalivyoainishwa.

Ni matumaini yetu pia kuwa kitabu hiki kitaongeza uelewa kwa wadau wote juu ya umuhimu wa kuikuza sekta hii muhimu na vile vile kujua kinachoendelea katika sekta ya madini kwa ujumla.

## Wajumbe wa Kamati:-

1. Mhe. Jaji Mark Bomani- Mwanasheria Mkuu Mstaafu na Wakili wa Kujitegemea
2. Mhe. John M. Cheyo – Mbunge Bariadi Mashariki
3. Mhe. Iddi M. Simba – Mbunge Mstaafu Ilala
4. Mhe. Dkt. Harrison Mwakyembe – Mbunge Kyela
5. Mhe. Zitto Zuberi Kabwe – Mbunge Kigoma Kaskazini
6. Mhe. Ezekiel M. Maige – Mbunge Msalala
7. Bw. David Tarimo – Mshauri wa Kodi, Kampuni ya PricewaterhouseCoopers
8. Bw. Peter L. Machunde – Mwenyekiti Soko la Hisa la Dar es Salaam
9. Bw. Mugisha G. Kamugisha – Kamishna wa Sera, Wizara ya Fedha na Uchumi
10. Bi. Maria Kejo – Mkurugenzi wa Madai na Sheria za Kimataifa, Wizara ya Katiba na Sheria
11. Bw. Edward D. Kihunrwa – Mkurugenzi Msaidizi, Udhibiti na Usimamizi wa Uendelezaji Mijo, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi
12. Bi. Salome Makange – Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wizara ya Nishati na Madini

## Sekretariati yenye wajumbe sita iliteuliwa kusaidia kazi za Kamati:-

1. Bw. Mathias B. Kabunduguru – Mkurugenzi wa Uendelezaji Sera, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma
2. Bw. Eliakim C. J. Maswi – Kamishna Msaidizi wa Bajeti, Wizara ya Fedha na Uchumi
3. Bi. Sarah Barahomoka – Mkurugenzi Msaidizi, Uandishi wa Sheria, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali
4. Dkt. Medard M. C. Kalemani – Wakili wa Serikali, Wizara ya Nishati na Madini
5. Bw. Shubi J. Byabato – Mjiolojia Mwandamizi, Wizara ya Nishati na Madini
6. Bw. Frank F. M. Lupembe – Afisa Kodi Mkuu, Mamlaka ya Mapato Tanzania.

# SURA YA KWANZA

## 1.1 Utangulizi

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilipitisha sera ya Madini mnamo mwaka 1997 kwa lengo la kuhakikisha kuwa sekta ya Madini inachangia ipasavyo katika pato la Taifa. Kufuatia kupitishwa kwa sera hiyo, Serikali iliwasilisha Bungeni Muswada wa Sheria ya Madini na kupitishwa mwaka 1998. Sheria hii ilikusudiwa kuweka misingi ya kisheria ya kufanikisha utekelezaji wa Sera ya Madini.

Takwimu zinaonyesha kuwa shughuli za uchimbaji mkubwa wa madini zimeongezeka kwa kuanzishwa migodi mikubwa sita mipya ya dhahabu kati ya mwaka 1997- 2007. Vile vile kumekuwa na ongezeko la shughuli za uchimbaji wa madini ya vito kama almasi na tanzanite. Aidha shughuli za uchimbaji madini zimeongezeka kutoka wachimbaji wenye leseni wapatao 2,000 mwaka 1997 na kufikia takribani wachimbaji 7,000 mwaka 2007. Takwimu pia zinaonyesha mchango wa sekta ya madini umeongezeka kutoka 1.7% mwaka 1997, na kufikia 3.8% mwaka 2006.

Miongoni mwa malalamiko ya wananchi ni pamoja na hali inayoonekana ya sekta ya madini kutochangia vya kutosha katika maendeleo ya nchi hasa ya kiuchumi na kijamii. Pia imeonekana kuwa mikataba ya madini inapendelea zaidi makampuni makubwa ya uwekezaji katika madini, huku kukiwepo na usiri mkubwa wa mikataba hiyo.

Katika siku za karibuni, malalamiko makubwa zaidi yamekuwa juu ya mfumo wa kodi ambapo kumekuwa na hisia kuwa kampuni za madini hazilipi kodi kiasi cha kutosha, huku kampuni zote zinazojishughulisha na uchimbaji wa dhahabu na almasi zikidai hazijapata mapato yanayostahili kulipa kodi. Aidha, kumekuwa na lawama kuhusiana na wananchi waliohamishwa kutoka maeneo yao ya asili ili kupisha uchimbaji mkubwa kutolipwa fidia ya ardhi zao. Pia wananchi wanaotoka wilaya zenye migodi wanalalamika kutopata sehemu ya mrahaba licha ya maisha yao kuathiriwa na shughuli za uchimbaji wa madini katika maeneo yao.

Baadhi ya kero za wananchi ni pamoja na zile za mazingira ambapo inasemekana kuwa mazingira yanaharibiwa sana. Vile vile wafanyakazi wa kitanzania katika migodi wanalalamika athari za kiafya wanazopata na ujira mdogo kulinganisha na wafanyakazi wageni.

Baadhi ya wananchi wanalalamikia udhaifu katika usimamizi wa sekta, yakiwemo masuala ya usafirishaji wa mchanga wa dhahabu nje ya nchi, kuchenjuliwa na kutotolewa kwa taarifa sahihi za gharama za uwekezaji na uzalishaji. Vile vile kumekuwapo malalamiko makubwa ya wananchi kwamba viongozi wao wanafaidika binafsi kutoka kwa wawekezaji, zikiwemo tuhuma za rushwa katika mikataba.

## 1.2 Kuundwa kwa Kamati

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania - Jakaya Mrisho Kikwete aliona umuhimu wa kutathmini upya mfumo wa usimamizi wa sekta ya madini kwa mapana zaidi ili kunufaisha taifa pamoja na wawekezaji. Rais alionyesha dhamira hiyo katika hotuba yake ya kwanza kulizindua Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mara baada ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005.

Aidha, Mheshimiwa Rais alirudia kauli yake wakati akifungua Mkutano Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi, tarehe 3 Novemba, 2007 mjini Dodoma. Tarehe 12 Novemba 2007, Rais aliteua Kamati aliyoahidi na kuipa miezi mitatu kukamilisha kazi yake.

## 1.3 Majukumu ya Kamati

Kamati hii ilipewa majukumu yafuatayo: -

1. Kupitia mikataba ya madini na nyaraka nyingine zinazohusu migodi mikubwa;
2. Kuchambua mfumo wa kodi unaotumika katika sekta ya madini;
3. Kupitia mfumo wa usimamizi unaofanywa na Serikali katika shughuli za uchimbaji mkubwa;
4. Kuchambua na kuainisha haki na wajibu wa mwekezaji na mwenye mali (Serikali);
5. Kukutana na Tanzania Chamber of Minerals and Energy" na wadau wengine ili kupata maoni yao;
6. Kutoa taarifa yenye mapendekezo.
7. Kupitia taarifa mbalimbali za Kamati zilizotangulia kuhusu sekta ya madini
8. Kumualika mtu yeyote mwenye utaalamu katika sekta ya madini ili kupata maoni yake; na
9. Kushauri juu ya mambo mengine yoyote yanayohusu sekta ya madini ambayo kamati itaona yanafaa.




## 1.4 Muundo wa Taarifa ya Kamati

Taarifa hiyo ina sura sita. Sura ya kwanza inahusu utangulizi. Sura ya Pili inaeleza hali halisi ya sekta ya madini; Sura ya tatu inaeleza maoni ya wadau mbalimbali; Sura ya nne inahusu uzoefu wa nchi nyingine katika kusimamia shughuli za madini; Sura ya tano inatoa tathmini, maoni na mapendekezo ya kamati; na Sura ya sita ni Hitimisho.

Taarifa hii fupi ya kamati inaainisha baadhi tu ya mambo muhimu yaliyoko katika taarifa halisi ya kamati ya Rais kuishauri Serikali kuhusu usimamizi wa sekta ya madini.

# SURA YA PILI

## 2.1 Hali halisi ya Sekta ya Madini

Katika Sura hii kamati inazungumzia kuhusu rasilimali ya madini na mchango wake katika maendeleo ya taifa, ambapo wameonyesha kulingana na kanzi data (data base) ya Wizara ya Nishati na Madini. Madini yanayoweza kupatikana nchini Tanzania yamegawanyika katika makundi matano:- Kundi la jamii ya madini ya metali linalojumuisha dhahabu, chuma, níkel, shaba, kobalti na fedha; kundi la jamii ya vito linalojumuisha almasi, tanzanite, yakuti, garnets na lulu; kundi la jamii ya madini ya viwandani linalojumuisha chokaa, magadi soda, jasi, chumvi na fosfeti; madini yanayozalisha nishati kama makaa ya mawe na uranium; na madini ya ujenzi kama vile kokoto, mchanga na madini kwa ajili ya terazo.

Mchanganuo wa hazina ya madini iliyothibitishwa nchini umeoneshwa katika jedwali Na.1 kama ifuatavyo:-

**Jedwali Na.1: Hazina ya Madini iliyothibitika**

| AINA YA MADINI | KIASI |
|---|---|
| Dhahabu | Tani 2,222 |
| Nikeli | Tani milioni 209 |
| Shaba | Tani milioni 13.65 |
| Chuma (Iron Ore) | Tani milioni 103.0 |
| Almasi | Karati milioni 50.9 |
| Tanzanite | Tani 12.60 |
| Limestone | Tani milioni 313.0 |
| Magadi soda (soda ash) | Tani milioni 109 |
| Jasi (gypsum) | Tani milioni 3.0 |
| Fosfeti (Phosphate) | Tani milioni 577.04 |
| Makaa ya mawe | Tani milioni 911.0 |

**Chanzo: Geological survey of Tanzania, 2007**

Pamoja na kuwepo hazina hii kubwa, Mchango wa sekta hii katika uchumi wa taifa na maendeleo ya jamii unaonekana kutokidhi matarajio ya wananchi ikilinganishwa na sekta nyingine za uchumi.

Kwenye mapitio ya sera ya madini imeonekana kuwa kufuatia umuhimu wa sekta ya madini Serikali ilipitisha Sera ya Madini ya Mwaka 1997. Madhumuni ya sera hii ni pamoja na kuchochea utafutaji na uendelezaji wa uchimbaji madini, kuboresha uchimbaji mdogo wa madini na kupunguza umaskini, kuimarisha miundombinu ya kijamii na kiuchumi, kuingiza fedha za kigeni na mapato kwa serikali, kukuza na kuiendeleza Tanzania kuwa kituo cha vito katika Afrika na kuhimiza usalama na uhifadhi wa mazingira.

Mwaka 1998, Serikali ilitunga sheria mpya ya madini na kuifanyia marekebisho Sheria ya Fedha za Kigeni (The foreign Exchange Act, 1992) ili kukidhi mahitaji ya sekta ya madini na kuzingatia Sera ya Madini ya 1997.

Ili kutekeleza sera hii sheria za kodi zimeweka vivutio mbalimbali kama ifuatavyo:-

### 2.1.1. Kodi ya Mapato

Sheria ya kodi ya mapato ambayo ndiyo inatumika hivi sasa katika utozaji wa kodi ya mapato ina vifungu maalum vinavyohusu utozaji wa kodi kwenye sekta ya madini.

Vifungu hivi ni kama kifungu cha 15(3) ambacho kinaruhusu fedha zinazokadiriwa kwa ajili ya kuhuisha mazingira kukombolewa na kampuni baada ya kutekeleza masharti. Kifungu cha 83(1)(a) kinazitaka kampuni kukata kodi ya zuio (witholding tax) kutoka kwenye malipo yaliyofanywa kwa ajili ya huduma za menejimenti za kitaalamu zilizotolewa kwa kampuni.

Hata hivyo baadhi ya vipengele vilivyokuwemo kwenye Sheria ya Kodi ya Mapato ya 1973 iliyofutwa bado vinaendelea kutumika katika ukadiriaji wa kodi ya mapato kwa ajili ya kampuni za madini. Kifungu Na. 145 cha Sheria ya Kodi ya Mapato ya 2004 kinaruhusu kutumika kwa sehemu ya tatu ya jedwali la pili la sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 1973 iliyofutwa.

Vipengele muhimu vinavyohusu utozaji wa kodi ya mapato na bado vinatumika ni pamoja na:-

I. Unafuu wa 100% wa gharama za uwekezaji katika ukokotoaji wa mapato yanayotozwa kodi kwa mwaka huo.

II. Unafuu wa ziada ya 15% ya gharama za uwekezaji. Kampuni zenye mikataba na serikali kwa ajili ya uwekezaji katika migodi **(Mining Development Agreements MDAs- Mikataba ya uendelezaji machimbo ya madini)**, iliyosainiwa kabla ya tarehe 1 Julai, 2001 zinaruhusiwa kukomboa ziada ya 15% ya gharama ya uwekezaji katika migodi. Unafuu huu wa ziada hutolewa kila mwaka.

    Athari kubwa ya kipengele hicho ni kampuni za madini kuchukua muda mrefu kabla ya kuanza kulipa kodi au kutolipa kabisa na hivyo kuinyima Serikali mapato yake.

III. Unafuu wa kodi unaotolewa katika ukokotoaji wa mapato ya kampuni za madini zinazoruhusiwa kukomboa gharama zote za uwekezaji na uendeshaji wa miradi yote wanayoendesha bila kujali kama miradi yote wanayoendesha inachangia katika mapato ya mwaka husika. Kwa utaratibu huo hakuna "ring fencing" kwa msingi wa mgodi kwa mgodi.

IV. Viwango vya kodi zuio (withholding taxes) vinavyotumika kwa kampuni zisizokuwa na MDAs au zile zilizoingia MDAs baada ya tarehe 1 Julai 2001 ni vile vilivyoainishwa kwenye Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2004. Viwango vya kodi ya zuio vinavyotumika ni vya sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 1973 iliyofutwa. Aidha, katika baadhi ya maeneo, viwango vilivyoainishwa kwenye Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 1973 havitumiki.




### 2.1.2 Kodi ya Ongezeko la Thamani (Value added Tax- VAT)

Kodi ya Ongezeko la Thamani inatozwa kwenye bidhaa na huduma zinazouzwa hapa nchini na zile zinazoingizwa kutoka nje. Sheria inayotumika kutoza kodi hii ni ***Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani*** Sura 148. Kwa mujibu wa Sheria hiyo watu na taasisi zilizoorodheshwa kwenye jedwali la tatu wanapata nafuu ya kodi ya VAT (VAT Relief).

Kwa mujibu wa aya ya 8, kampuni za madini hazipati nafuu ya VAT kwenye bidhaa ambazo zimeingizwa kutoka nje ya nchi pia hawapati msamaha wa ushuru wa Forodha.

### 2.1.3 Ushuru wa Forodha

Kampuni za madini na wakandarasi wao zinapata msamaha wa ushuru wa forodha kutegemea hatua iliyofikiwa katika shughuli za madini kama ifuatavyo;-

I. Katika kipindi cha utafutaji, ujenzi wa migodi kabla ya kuanza uzalishaji mpaka kukamilika kwa mwaka wa kwanza wa uzalishaji, kampuni za madini pamoja na wakandarasi wao zinaruhusiwa kuingiza nchini bidhaa mbalimbali zinazohusiana na shughuli za madini bila kulipia ushuru wa forodha. Bidhaa hizo ni pamoja na mitambo, baruti, vipuri, magari, mafuta na vilainishi (lubricants). Hata hivyo, msamaha huo hutolewa na kamishna wa forodha kwa kushauriana na waziri mwenye dhamana ya madini na kuridhika kuwa vifaa hivyo vitatumika kwa shughuli za madini.

II. Baada ya mwaka wa kwanza wa uzalishaji, kampuni na wakandarasi hutakiwa kulipa ushuru wa forodha kwa kiwango kisichozidi 5% kwenye mitambo, baruti, vipuri, magari, mafuta na vilainishi badala ya viwango vya jumla vya ushuru wa forodha kwa bidhaa zinazoingia katika eneo la Jumuiya ya Afrika Mashariki (Common External Tariff - CET). Kwa mfano, kiwango cha ushuru wa forodha kwenye baruti ni 10% lakini kampuni za madini na wakandarasi wanalipa ushuru kwa kiwango cha 5%.

### 2.1.4 Ushuru wa Bidhaa

Kampuni za madini zimesamehewa ushuru wa bidhaa kwenye mafuta zinayoingiza toka nje au kununua ndani kwa shughuli za uzalishaji wa Madani. Hii ni kwa mujibu wa Tangazo la Serikali No. 480 lililochapishwa tarehe 25 Oktoba 2002.

### 2.1.5 Ushuru wa Mafuta

Ushuru wa mafuta hutozwa chini ya "The Road and Fuel Act", Chapter 220. Kampuni zinazozalisha madini ya dhahabu na ambazo zimo kwenye makubaliano ya uendelezaji madini zimesamehewa ushuru wa mafuta unaozidi dola za Marekani 200,000 kwa mwaka. Msamaha huu ni kwa muda wote wa MDA (mikataba ya uendelezaji machimbo ya madini) au maisha ya mgodi kwa kutegemea chochote kitakachotokea. Hii ni tofauti ambapo msamaha huo ulikuwa kwa mwaka wa kwanza tu kama ilivyoainishwa na tangazo la serikali No. 22 la 1999 ambalo lilifutwa na tangazo la serikali no. 99 la tarehe 15 Octoba, 2005. Kampuni zinazojihusisha na madini mengine na wachimbaji wadogo hazipati msamaha huu.

### 2.1.6 Ushuru wa Stempu

Kampuni za Madini zenye MDA hutumia viwango vya ushuru wa stempu vilivyotajwa kwenye MDA husika, ambavyo ni vidogo kulinganisha na Jedwali la kwanza la Sheria ya Ushuru wa Stempu Sura 189 wakati mikataba iliposainiwa.

### 2.1.7 Kodi za Serikali za Mitaa

Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa inazitaka kampuni zote pamoja na kampuni za madini kulipa kwenye Halmashauri husika 0.3% ya mauzo yote. Hata hivyo, MDA zimeweka kiwango cha juu cha dola za Marekani 200,000 kwa mwaka.

## 2.2 Mikataba ya Madini:

Kati ya mwaka 1994- 2007, mikataba ya Madini sita imesainiwa, yote ikiwa ni ya migodi mikubwa ya dhahabu. Migodi hiyo na mikataba ni: - Bulyanhulu uliosainiwa tarehe 5 Agosti 1994; Golden Pride ulioko Nzega uliosainiwa tarehe 25 Juni 1997; Geita Gold Mine uliopo Geita uliosainiwa tarehe 24 Juni 1999; North Mara uliopo Tarime uliosainiwa tarehe 24 Juni 1999; Tulawaka uliopo Biharamulo uliosainiwa tarehe 29 Desemba 2003; Buzwagi uliopo Kahama uliosainiwa tarehe 17 Februari 2007. Kwa mujibu wa kifungu cha 10(1) cha sheria ya Madini, waziri mwenye dhamana ya madini ndiye mwenye mamlaka ya kuingia katika mkataba wa uendelezaji wa mgodi na mwekezaji kwa niaba ya serikali. Mambo muhimu anayopaswa kuzingatia yametajwa kwenye kifungu cha 10(2) ikiwa ni pamoja na:-

- Kuwepo na mfumo wa kodi usiobadilika (fiscal stability) kwa kipindi chote cha mradi;
- Namna waziri au kamishna anavyoweza kutumia madaraka yake kutekeleza mkataba;
- Kuainisha ukomo wa wajibu wa mwekezaji katika uhifadhi mazingira;
- Namna ya kushughulikia migogoro inayoweza kutokea na Mining Development Agreements (Mikataba ya Uendelezaji Machimbo ya Madini) husika.

Pamoja na mambo yaliyoainishwa kwenye sheria ya Madini mambo mengine yaliyomo kwenye MDA's ni pamoja na kampuni kuruhusiwa kuweka fedha nye ya nchi na kuweka ukomo wa tozo za Halmashauri na Serikali za Mitaa.

## 2.3 Matatizo ya wachimbaji wadogo:

Baadhi ya malalamiko yamekuwa yakitolewa na wachimbaji wadogo ikiwemo kunyang'anywa maeneo yao na wachimbaji wakubwa kwa msaada wa Serikali kwa kutumia vyombo vya dola kama vile polisi. Maeneo madogo wanayopewa yanakuwa na matatizo ya kuchimba bila kuingiliana, kwa mfano Mirerani ambako eneo walilotengewa wachimbaji wadogo ni mita 50x50 ukilinganisha na Kitalu C walilopewa wachimbaji wakubwa. Vile vile wachimbaji wadogo wamejikuta wakifanya kazi katika mazingira ya hatari na yasiyo salama ikiwemo kutobozana na ajali za mara kwa mara kama ilivyotokea mwezi Machi, 2008.

Imeelezwa pia kuwa inapotokea wachimbaji wadogo wametoboa mgodi wa mwekezaji mkubwa wamekuwa wakipigwa, kuteswa kwa kuumwa na mbwa, kumwagiwa maji na hata kupigwa risasi na mchimbaji mkubwa. Wachimbaji wadogo wamelalamika kuwa Serikali haiwajali kwa kutowawekea mazingira ya kupata mitaji, ushauri wa kitaalamu, na masoko ya mazao yao. Na pia ilielezwa kuwa hawapati misamaha ya kodi kama ilivyo kwa kampuni za uchimbaji mkubwa.



# SURA YA TATU

## 3.1 Maoni ya wadau:

Ili kubaini  na kuandaa mapendekezo ya jinsi ya kuondoa upungufu unaosababisha malalamiko kuhusu sekta ya madini, kamati ilikutana na wadau mbalimbali wakiwemo wenye migodi, wafanyabiashara ya madini, wafanyakazi migodini, wataalamu wa sekta ya madini na wananchi kwa ujumla wao.

Kamati ilikutana na uongozi wa migodi ambao ulionesha kuridhishwa na mazingira ya uwekezaji katika sekta ya madini hapa nchini. Viongozi hao walisisitiza umuhimu wa kuwa na mahusiano mazuri baina yao na jamii inayowazunguka, na kuieleza kamati kuwa suala la uhusiano mzuri na jamii mwenyeji ni sehemu muhimu ya sera zao za kuendesha biashara. Uongozi wa migodi ulipendekeza mabadiliko katika maeneo mbalimbali kama vile:-

1. Utaratibu wa utoaji leseni na vibali vya uchimbaji wa madini, ambapo uongozi huo ulionesha kutoridhishwa na utendaji kazi wa taasisi mbalimbali za Serikali zinazowahudumia. Pia ucheleweshaji wa utoaji leseni za utafutaji uchimbaji wa madini katika Ofisi za Waziri na Kamishna wa Madini ambao ndiyo wenye mamlaka ya utoaji leseni hizo; vile vile Wizara ya Kazi na Maendeleo ya Vijana kuchelewa kutoa vibali vya ajira kwa wafanyakazi wa kigeni; Idara ya Uhamiaji kuchelewa kutoa vibali vya kuishi kwa wafanyakazi wa kigeni; na Mamlaka ya Mapato kuchelewesha marejesho ya VAT na kutokamilisha kwa wakati taratibu za misamaha au nafuu ya kodi kwa kampuni za madini.
2. Serikali kutotimiza majukumu yake; serikali imeshindwa kudhibiti wachimbaji wadogo na wananchi wanaovamia maeneo ya migodi, na hivyo kusababisha migongano baina ya migodi na wachimbaji wadogo.
3. Uhaba wa wataalamu katika sekta ya madini; Serikali haijafanikiwa ipasavyo katika kuhakikisha kuwa Taifa linajitosheleza kitaaluma katika sekta ya madini na ndiyo sababu ya wawekezaji kutafuta wataalamu kutoka nchi za nje. Pia wenye migodi walilalamikia ukosefu wa uzoefu wa kutosha kwa wataalamu wa hapa nchini kutokana na sekta yenyewe kuwa changa. Wataalamu wachache wanaopata uzoefu kuondoka kwenda kufanya kazi nchi za nje pia ni tatizo.
4. Udhibiti wa ufuatiliaji wa vitendo vya uhalifu;
5. Fidia kwa wananchi wanaopisha migodi;
6. Uduni wa miundombinu;
7. Rushwa Serikalini;
8. Ulipaji wa mrabaha;
9. Ongezeko la gharama za ajira;
10. Uhusiano kati ya wawekezaji na jamii;
11. Ununuzi wa bidhaa na huduma za ndani;
12. Uwezo mdogo wa mamlaka ya mapato (TRA) katika kuhudumia sekta ya madini;
13. Athari za kiafya kutokana na ajira migodini; viwango vya fidia kwa wafanyakazi wanaoumia kazini kwa sasa ni vidogo sana;
14. Ushirikishwaji wa wananchi katika ugawaji wa maeneo ya uchimbaji;
15. Uwazi katika mikataba ya madini kati ya Serikali na wawekezaji; kuna usiri mkubwa kuhusu mikataba ya uchimbaji wa madini.

16. Udhibiti wa madini wananchi, walionyesha wasiwasi juu ya uwezo wa Serikali katika kudhibiti madini kwa vile wasimamizi wa madini wanakaa mbali na migodi, hali hii inaruhusu uwezekano wa madini kutoroshwa, jambo ambalo linaweza kupelekea upotevu wa mapato ya Serikali.

17. Utunzaji wa mazingira, ilielezwa kuwa hakuna utaratibu wowote wa fidia kwa ajili ya mazao ya wanakijiji au athari nyingine wanazopata.

Kamati ilipata wasaa wa kujadiliana na wataalamu mbalimbali ambao nao walielezea matatizo mbalimbali yanayojitokeza pamoja na mapendekezo;

1. Akiba ya madini; ni maoni ya Taifa kutunza akiba ya madini ambayo tayari yamechimbwa na kuchenjuliwa na kuhifadhiwa katika hali ya kuwa tayari kwa matumizi au kuuzwa pale itakapolazimu.
2. Matumizi ya mapato yatokanayo na madini hayajulikani vizuri na hivyo kujenga hisia kwamba Taifa halinufaiki na madini.
3. Mfumo wa kodi.
4. Mrabaha.
5. Ushiriki wa kampuni za madini katika maendeleo ya jamii, wananchi wengi hawaridhishwi na kiwango cha mchango wa kampuni katika maendeleo yanayopatikana katika maeneo ya migodi hiyo.

# SURA YA NNE

## 4.1 Tathmini, maoni na mapendekezo ya kamati.

Katika sura hii kamati imeonyesha uchambuzi wa maoni ya wadau ambao unaonesha mitazamo tofauti kama ifuatavyo:-

- Mfumo wa usimamizi wa sekta ya madini, wawekezaji wangependa uboreshwe kwa kuimarisha miundombinu, huduma za usalama na usimamizi wa kodi;
- Wananchi wanaoishi karibu na migodi ambao huwa hawafaidiki na uvunaji wa rasilimali ya madini, wangependa kuona manufaa zaidi katika huduma za jamii na ajira kuliko ilivyo hivi sasa;
- Wachimbaji wadogo nao wanaona kuwa ujio wa uwekezaji umewasababishia wao kunyang'anywa maeneo yao na kuwapotezea fursa za kujipatia kipato na ajira kwa watu wengi.
- Wataalamu wa fani mbalimbali wazalendo wanaotoa huduma kwenye sekta ya madini wanaona kuwa serikali haijawawezesha katika kuisimamia kikamilifu sekta ya madini, kutokana na kutopatiwa mafunzo, nyenzo na bajeti ya kutosha;
- Vivutio vingi vilivyotolewa kwa wawekezaji ni matokeo ya mapungufu yaliyomo kwenye sera, sheria na mikataba inayosimamia na kuongoza sekta ya madini; na
- Serikali nayo hairidhishwi na namna sekta hii inavyochangia mapato yake na uchumi kwa ujumla.

Wadau wote wana maoni kuwa utaratibu mzima wa kuiendeleza sekta ya madini unahitaji kuangaliwa upya na kuboreshwa zaidi ili sekta hiyo iweze kukidhi matarajio ya Taifa.

Pamoja na hayo yote kuna masuala yanayojitokeza katika sekta ya madini ambayo yanahitaji kupatiwa ufumbuzi ili kuiboresha Sekta hiyo;

### 4.1.1 Wajibu wa Serikali na mwekezaji; Mapendekezo:-

- Kila sehemu yanapogundulika madini yenye kuhitaji uwekezaji mkubwa, Serikali ijenge miundombinu kama barabara, umeme, maji na huduma za jamii kama vituo vya afya, shule na huduma za usalama;
- Kwa mradi mkubwa kama Kabanga, Serikali ianze mapema maandalizi ya kuweka miundombinu ya umeme, barabara na reli;
- Serikali iwalazimishe wawekezaji kuwakatia bima za ajali wafanyakazi wao.

### 4.1.2 Sera ya Madini ya mwaka 1997; Mapendekezo:-

- Serikali iainishe na kuweka uwiano baina ya vivutio vya mfumo wa kodi na vingine kama vile, uwepo wa Madini na utulivu wa kisiasa
- Sera iainishe bayana nafasi ya serikali kushiriki katika uwekezaji kwenye sekta ya Madini.
- Sera iweke wazi umuhimu wa kushirikiana na kufungamanisha sekta ya madini na sekta nyingine za uchumi kama njia ya kuharakisha maendeleo; na
- Sera ielekeze vivutio vingi vitolewe kwa utafutaji wa madini na siyo kwa uchimbaji madini.

### 4.1.3 Mapendekezo mengine kwenye Sheria ya Madini:-

- Maombi ya leseni ndogo yawasilishwe katika ngazi za chini na leseni zitolewe katika ofisi za kanda ili kuharakisha shughuli za uchimbaji;
- Leseni za uchimbaji mkubwa (SML) zitolewe kulingana na mashapo;
- Utaratibu unaotumika sasa wa upokeaji hadi utoaji wa leseni kwa ujumla ni mzuri uendelee;

### 4.1.4 Mamlaka ya Waziri kufuta Leseni; Mapendekezo:-

- Kamati imependekeza kuwa Kifungu Na. 57 kifanyiwe marekebisho ili kumtaka Waziri atekeleze uamuzi wake ndani ya siku 60 baada ya kutoa taarifa ya kusudio la kufuta leseni.

### 4.1.5 Mamlaka ya Waziri kuingia mikataba; Mapendekezo:-

- Kamati imependekeza Kifungu cha 10 cha Sheria ya Madini kifanyiwe marekebisho kwa kumtaka Waziri mwenye dhamana ya kuingia mkataba wa madini kufanya mashauriano kwanza na mamlaka husika katika maeneo ya mgodi husika kabla ya mkataba.



### 4.1.6 Kamati ya ushauri ya madini (MAC):-

Kwa mujibu wa Kifungu Na. 20 Kamati hiyo ni ya ushauri tu ambapo Waziri anaweza kutofuata ushauri huo.

**Mapendekezo:**

- Kamati imependekeza kuwa, mara baada ya kuanzishwa mamlaka ya Madini inayopendekezwa katika taarifa hii, Kamati ya ushauri wa madini ivunjwe na majukumu yake yatakayokuwa yameboreshwa yahamie kwenye Mamlaka hiyo.

### 4.1.7 Masuala ya Fidia; Mapendekezo:-

- Kamati imependekeza kuwa, Sheria ya Madini ifanyiwe marekebisho kwa kujumuisha vipengele vya fidia kwa wanaopisha shughuli za madini.




### 4.1.8 Utatuzi wa migogoro; Mapendekezo:-

- Kamati imependekeza kuwa; Kifungu cha 101(2) cha Sheria ya Madini kirekebishwe ili kumtaka Kamishna kutatua migogoro iliyowasilishwa kwake au kutoa sababu za kukataa kusikiliza mgogoro huo; na
- Liundwe baraza maalum kwa ajili ya kutatua migogoro ya madini (Mining Tribunal).

### 4.1.9 Utozaji wa Mrabaha; Mapendekezo:-

- Kamati inapendekeza kuwa tozo la mrabaha lizingatie ukokotoaji kwa kigezo cha gross value Badala ya net back value.

### 4.1.10 Usimamizi wa sekta ya madini; Mapendekezo:-

- Ianzishwe mamlaka ya madini nchini inayojitegemea na iwe na jukumu la kusimamia na kuendeleza sekta.
- Mamlaka hiyo ipewe wataalamu wenye ujuzi na uzoefu katika sekta ya madini na vitendea kazi na bajeti ya kutosha;
- Mamlaka hiyo ipewe sehemu ya makusanyo ya mrabaha kwa ajili ya bajeti yake;
- Kitengo cha uwekezaji na uendeshaji katika migodi mikubwa kiimarishwe kwa kuongezewa wafanyakazi, vitendea kazi na sehemu ya kufanyia kazi ili kuweze kufanya shughuli zake kikamilifu.
- Kuhusu suala la Tansort, Kamati inakubaliana na lengo la Serikali la kukirejesha kitengo hicho nchini na kupendekeza kuwa, kiimarishwe ili kiweze kuchambua almasi zote zinazozalishwa nchini.

### 4.1.11 Uzoefu wa umiliki na ushiriki wa Serikali :-

Serikali inahusika katika kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji na kuiachia sekta binafsi kuwekeza katika shughuli za uchimbaji madini.

#### Mapendekezo kwa Migodi:-

- **Mgodi wa Buhemba**
  - Serikali ifanye uchunguzi wa kina juu ya uanzishwaji wa kampuni za Meremeta na Tangold, umiliki wa Serikali katika kampuni hizo na uhalali wa malipo ya dola za Marekani milioni 132 yaliyofanywa na Benki Kuu kwa Benki ya Nedbank ya Afrika Kusini.
  - Serikali ichukue jukumu la kuhakikisha mgodi unafungwa kwa kuzingatia sheria na taratibu za ufungaji mgodi.
  - Serikali iharakishe kufanya malipo ya madai ya wafanyakazi ya Tsh. 282 milioni; na
  - Serikali ithamini madai yote ya wananchi wa Buhemba ikiwemo uharibifu wa miundombinu ya huduma za jamii, na kufanya ukarabati stahili.
- **Mgodi wa Bulyanhulu**
  - Kamati inapendekeza kuwa, kabla ya kuamua kuachia au kuuza hisa zake kwenye kampuni za migodi, Serikali ifanye tathmini yakinifu kuzingatia manufaa kwa taifa na malengo ya muda mrefu.
- **Mgodi wa Kiwira**
  - Serikali ichukue hatua za haraka kuchunguza uhalali wa taratibu zilizotumika za kubinafsisha mgodi huo, malalamiko ya wafanyakazi ya kupunjwa mafao yao na uchafuzi wa mto Kiwira;
  - Serikali ichunguze uhalali wa matumizi ya shilingi bilioni 13 kwa ajili ya kukarabati mgodi na uzalishaji; na
  - Serikali ichunguze madai ya uuzwaji wa mali za mgodi na utekelezaji wa masharti ya ubia.

- **Mgodi wa Mwadui**
  - Mapato ya mgodi huu mwaka 1994 ilikadiriwa kuwa dola za Marekani bilioni 4.8. Kuna umuhimu wa Serikali kuendelea na umiliki wa hisa hizo kwa 25% badala ya kukubali pendekezo la WILCROFT kuuza hisa 20% na kubakiza 5% tu;
  - Serikali ianzishe utaratibu wa kiushindani wa uuzaji wa almasi zinazozalishwa katika mgodi wa Mwadui;

### 4.1.12 Mgawanyo wa mapato yatokanayo na madini:

Kamati imebaini kuwa hakuna utaratibu wa kufanya mgawanyo maalum kwa ajili ya mapato yatokanayo na madini. Jambo hili linaleta wasiwasi na hisia tofauti kuhusu matumizi halisi ya mapato haya na manufaa yake kwa taifa na wananchi kwa ujumla.

#### Mapendekezo:-

- Katika mgao wa mrabaha 60% iende kwenye mfuko wa maendeleo ya madini kwa ajili ya miradi endelevu;
- 20% ya mrabaha iende kwenye mamlaka ya madini inayopendekezwa kuundwa katika taarifa hii;
- 10% iende wilaya yenye mgodi;
- 7% iende wilaya yenye mgodi;
- 7% iende kwenye Halmashauri nyingine katika mkoa wenye mgodi;
- 3% iende kwenye vijiji vinavyozunguka mgodi.

### 4.1.13 Mikataba ya madini;

Baada ya kuipitia mikataba ya madini, kamati imebaini maeneo muhimu ya utatuzi wa migogoro, mfumo wa kodi, masharti kuhusu Fedha za kigeni, wafanyakazi wa kigeni na ubadilishaji wa umiliki.

#### Mapendekezo:-

- Kuwepo mfumo imara wa sheria utakaofanya uwekezaji katika shughuli za madini ufanyike kufuatana na sheria za nchi zinazosimamia uwekezaji kwa ujumla badala ya mikataba maalum na mwekezaji mmoja mmoja;
- Mikataba binafsi iruhusiwe pale tu ambapo uwekezaji ni wa kiwango cha dola za Marekani milioni 200 au zaidi;
- Mikataba itakayoingiwa ni lazima ipelekwe Bungeni kwa taarifa;
- Sheria ya madini ifanyiwe marekebisho ili iweke vipengele vyote muhimu vinavyohusu uwekezaji katika sekta ya madini ili kuwa na Sheria inayojitosheleza;
- Mikataba iwe wazi kwa wananchi na ipatikane katika ofisi za mikoa, wilaya na Halmashauri ambapo migodi iko;
- Mikataba yote haifanani. Mikataba yote ifanane na kwa ajili hiyo kuwe na model agreement ambayo itakuwa sehemu ya Sheria ya Madini;
- Msamaha wa ushuru wa mafuta isipokuwa kwa mafuta yatakayotumika kwa uzalishaji wa umeme unaotumika migodini tu;
- Gavana aachiwe nafasi ya kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria;

- 60% ya fedha inayotokana na mauzo ya madini irejeshwe nchini kwa ajili ya matumizi ya ndani;
- Mikataba iweke vipengele vinavyomlazimisha mwekezaji kununua bidhaa na huduma zinazopatikana hapa nchini ili mradi ziwe na ubora unaofaa;
- Mkataba uwatake wafanyakazi wa kigeni wanapoingiza gari na vifaa vingine kulipa ushuru na kodi nyingine kwa mujibu wa sheria husika kama ilivyo kwa wafanyakazi wa sekta nyingine; na
- Viwango vya ushuru wa stempu vilivyowekwa kwa mujibu wa Sheria vilipwe kama ilivyokuwa wakati wa kuingia mikataba hiyo.

### 4.1.14 Ulipaji wa fidia;- Mapendekezo:-

- Utaratibu wa ulipaji fidia kwa wanaopisha shughuli za madini uwekwe kwenye Sera na ufafanuliwe kwenye Sheria ya Madini. Aidha Sheria ya Madini iweke masharti kwa ulipaji wa fidia uambatane na upatikanaji wa makazi mapya na ujenzi wa miundombinu katika makazi hayo. Sheria itamke bayana mwenye jukumu la kulipa fidia kuwa ni mwekezaji ambaye atajumuisha gharama hizo katika gharama za mgodi.

### 4.1.15 Wachimbaji wadogo; Mapendekezo:-

- Muda wa leseni ndogo za uchimbaji uongezwe kufikia miaka kumi(10) ili kuwawekea mazingira mazuri zaidi ya kupata mitaji kutoka kwenye taasisi za Fedha.
- Wachimbaji wadogo wasaidiwe mbinu kwa ajili ya kupata mtaji wa ununuzi wa vitendea kazi;
- Serikali ikubali kuchangia mfuko maalum kwa ajili ya mitaji na mikopo kwa wachimbaji hawa;
- Kuanzishwe taasisi za fedha kwa ajili ya mikopo kupitia SACCOS zao;
- Serikali iweke utaratibu wa kisheria utakaowalazimu wawekezaji kuwakatia bima za ajali wafanyakazi wao.



### 4.1.16 Mchango wa Sekta ya Madini katika Maendeleo na huduma za jamii (Corporate Social Responsibility); Mapendekezo:-

- Ni vyema wawekezaji wakapewa nafasi ya kushiriki katika kamati ya mashauriano ili wajue vipaumbele vya huduma zinazohitajika;
- Wawekezaji washauriwe kutoa huduma kwa jamii ili kuimarisha mahusiano mazuri;
- Sehemu ya mrabaha inayokwenda katika Halmashauri na wilaya zilizo na migodi, zitumike kuboresha huduma za jamii.

### 4.1.17 Ajira na rasilimali watu;

Maandalizi ya wataalamu yanayopaswa kufanywa na Serikali kwa mujibu wa Sera ya Madini ya Mwaka 1997.

### Mapendekezo:-

- kutokana na kutojitosheleza kwa wataalamu wa Madini, theluthi moja ya ada ya mafunzo inayolipwa na kampuni za Madini ambayo kwa kiasi kikubwa inatumika kuendeleza utaalamu wa sekta ya madini, itolewe kwa Mamlaka ya Madini itakayokuwa na jukumu la kusimamia uendelezaji wa taaluma za madini nchini.
- Serikali pia iwahimize wananchi kuepuka vitendo vya uhalifu ili kujenga mahusiano na kuaminiana na wawekezaji;
- Serikali iondokane na upendeleo wa kodi kwa wafanyakazi wa kigeni kwa kuwa unaikosesha mapato;
- Vibali vya ajira kwa wageni vitolewe tu pale inapobainika kuwa kuna mahitaji na pia utaalamu huo haupatikani hapa nchini;
- Serikali ihakikishe wawekezaji wanatii sheria za nchi; na
- Wawekezaji waelimishwe kwamba kuheshimu mifumo rasmi ya utatuzi wa migogoro ni kwa faida yao pia, na siyo kwa faida ya wafanyakazi tu.

### 4.1.18 Biashara ya madini; Mapendekezo:-

- Kwa kuwa hakuna utaratibu maalum wa kuuza na kununua madini, Serikali iweke utaratibu wa biashara ya madini na kusimamia ili kuepusha utoroshwaji wa madini na kupoteza mapato yake;
- Kwa kuwa madini yaliyokatwa yana thamani kubwa kuliko yasiyokatwa, kuna umuhimu wa Serikali kuhamasisha na kuwezesha wafanyabiashara wafanye shughuli za ukataji wa madini;
- Serikali iwe na utaratibu wa kuandaa maonesho ya vito na kuanzisha kituo cha minada ya vito; na
- Kuwe na udhibiti mzuri wa madini ya vito yanayozalishwa nchini ili kuweza kuwavutia wawekezaji katika usanifu wa vito.
- Kuwe na kitengo maalum katika Mamlaka itakayoundwa kwa ajili ya kusimamia biashara ya madini ya vito na almasi.

### 4.1.19 Usimamizi wa mazingira; Mapendekezo:-

- Kamati imependekeza kuwa Kanuni ya 31 Kanuni za Uchimbaji (Usimamizi na Ulinzi wa Mazingira) ya 1999 ifanyiwe marekebisho na kumtaka Waziri kuingia mkataba na kila kampuni yenye leseni ya uchimbaji wa kati na mkubwa na kuzilazimisha kampuni hizo kutenga fedha halisi au kuwa na dhamana kamili kwa ajili ya kurekebisha mazingira.

- Wachimbaji wadogo wapewe elimu kuhusu uhifadhi wa mazingira na matumizi bora ya madawa ya kusafishia madini, hasa zebaki;
- NEMC na Mamlaka ya Madini itakayoundwa ziimarishwe ili ziweze kusimamia mazingira katika sekta ya madini.




### 4.1.20 Uchenjuaji na usafishaji madini; Mapendekezo:-

- Serikali iweke mikakati katika Sera ya Madini na kutunga au kurekebisha Sheria ya Madini kuingiza vipengele vitakavyowezesha uanzishwaji na uimarishwaji wa shughuli za uchenjuaji na usafishaji wa madini hapa nchini.

## 4.2 Fungamanisho la sekta ya madini na uchumi;

### Mapendekezo:-

- Sekta zenye uhusiano wa moja kwa moja na uchimbaji wa madini kama vile miundombinu ya barabara, reli, na bandari, sekta ndogo ya umeme, maji, ziimarishwe ili zinufaike na ukuaji wa sekta hii ya madini;
- Shirika la Umeme Tanzania- TANESCO iwezeshwe kufikisha na kuuza umeme kwa migodi yote iliyopo na itakayoanza baadaye;
- Mfumo wa reli ya kati uimarishwe ili kuweza kukidhi mahitaji ya sekta ya madini;

## 4.3 Fungamanisho la sekta ya madini na sekta ndogo ya umeme. Mapendekezo:-

- Vyanzo vya umeme vyenye gharama nafuu kwa mfano Stieglers' Gorge, Kiwira, Mchumchuma, na Ruhudji viendelezwe kwa umiliki au usimamizi wa TANESCO ili matumizi yake yazingatie uendelezaji wa sekta ya madini.

# SURA YA TANO

## 5.1 Hitimisho

Kamati ya taarifa hii, imehitimisha kazi yake kwa kusema yafuatayo: -

1. Nchi yetu Tanzania imebarikiwa neema ya madini ya aina mbalimbali yaliyo nchini pote. Kwa hiyo sekta hii ni muhimu sana katika uchumi wa taifa na inastahili kupewa kipaumbele na Serikali. Sheria, mikataba na taratibu za usimamizi wa shughuli za madini baadaye lazima zitofautiane na hizo za sasa, vivutio vya kodi katika kuwavutia wawekezaji si sahihi.

2. Serikali kumiliki hisa ndogo kama kwa kampuni ya Williamson Diamonds Limited ambapo Serikali ina hisa 25%, hali ambayo si sawa kwa umiliki wa kigeni.

   Upo umuhimu wa ushiriki wa kutosha wa watanzania katika umiliki wa hisa za kampuni za uchimbaji mkubwa.

   Shughuli zote za uchimbaji wa vito, na Kampuni za uchimbaji wa kati wa madini mengine, zimilikiwe ama kwa 100% au kwa kiasi kisichopungua 50% na wananchi wa Tanzania.

   Shughuli zote za wachimbaji wadogo zimilikiwe na kuendeshwa na watanzania tu.

3. Sekta ya madini itatoa faida stahili kwa wananchi pale tu itakapofungamana na uchumi mpana.

4. Serikali ihakikishe maeneo yote ya uchimbaji kwa hivi sasa yanafikishiwa miundombinu ya umeme, barabara, na maji.

   Kuwe na utaratibu wa ujenzi wa makazi mbadala kwa wananchi wanaohama kupisha shughuli za uchimbaji.

   Serikali ifikirie kujiunga na chombo kinachoitwa “Extractive Industries Transparency Initiative” (EITI) ambacho kimekwishavutia nchi kadhaa kama vile Ghana, Nigeria na kampuni kubwa za uchimbaji, jambo hili linahakikisha kwamba uwekezaji katika miradi ya mali asili zinazokwisha unafanyika kwa uwazi.

5. Hatua za haraka zichukuliwe na serikali katika kutekeleza yatakayoamuliwa.

   Vile vile kwa kadri ya uwezo, ni ushauri wa kamati kuwa taarifa hii na maamuzi ya Serikali vyote viwili, viwekwe wazi ili wananchi wafahamu kinachoendelea katika sekta hii muhimu nchini.

   Maeneo yanayostahili kipaumbele katika utekelezaji yametajwa kuwa;

   (a) Suala la maisha ya wananchi walioathirika vibaya na shughuli za madini hususan baada ya kuingia kwa wawekezaji wakubwa linastahili kushughulikiwa haraka sana. Kutolipwa fidia stahili, kutopatiwa makazi mbadala na kutopangiwa utaratibu wa ujirani mwema, kumezua migogoro mikubwa inayoondoa amani na usalama katika migodi.

   (b) Malipo ya madai ya wafanyakazi wa migodi ya Buhemba na Kiwira yafanyike haraka.

   (c) Kubadilisha msingi wa utozaji wa mrabaha badala ya kutoza kwenye ‘net back value’ utozwe kwenye ‘gross value’ na kuongeza viwango kutoka 5% kwa almasi na madini hadi 7% kwa madini ya vito, na kutoka 3% hadi 5% kwa madini ya metali ikiwemo dhahabu.

# MKAKATI WA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YALIYOMO KWENYE TAARIFA HII

Kamati inashauri kiundwe kikundi Kazi (Task Force) kitakachosimamia na kuratibu utekelezaji wake. Wajumbe wa kikundi hicho watoke katika wizara na taasisi zinazosimamia masuala haya. Itafaa sana kikundi kazi hiki kiongozwe na Afisa wa ngazi ya juu kutoka Ofisi ya Rais au Waziri Mkuu.



# Ripoti ya Bomani




**Taarifa fupi ya Kamati ya Rais ya Kuishauri Serikali kuhusu**

## Usimamizi wa Sekta ya Madini




policy forum

270 Kiko Avenue,
off Old Bagamoyo Road.
Mikocheni B,
P. O. Box 38486.
Tel/Fax: 2772611. Mobile: +255 782 317434
Dar es Salaam
Email: info@policyforum.or.tz
www.policyforum.or.tz

ISBN
9 789987 915736

Designed and Printed by The Print Factory